# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

## HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUDUMU YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI YA RAIS – KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

---

**Mheshimiwa Spika,** Awali ya yote napenda kutumia fursa hii adhim kumshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehma, Muumba wa mbingu na ardhi pamoja na vilivyomo kwa kutujaalia afya njema, kutupa pumzi na uhai kwani hii ni rehma kubwa aliyotujaalia ambayo wengine amewanyima. Pia napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi ya kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kwa lengo la kutoa maoni ya Kamati yangu ya Kudumu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha, 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** vile vile, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuiongoza nchi yetu kwa uadilifu, hekima na busara ambapo kumepelekea kupatikana kwa maendeleo pamoja na kuendelea kudumu kwa amani na utulivu katika nchi yetu.

**Mheshimiwa Spika,** shukuraani za pekee zimwendee Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais – Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Mwalim Haroun Ali Suleiman kwa ushirikiano wake mkubwa anao utoa kwa Kamati ambao

unatoa ufanisi katika kutekeleza majukumu yetu, Lakini pia, shukrani za dhati zimuendee, Katibu Mkuu Nd. Mansura Mossi Kassim, Naibu Katibu Mkuu Nd. Omar Haji Gora na Afisa Mdhamin Pemba, Ndugu Halima Khamis Ali pamoja na watendaji wote wa Ofisi hii kwa kushirikiana nasi katika kazi hizi za Kamati ikiwemo ya kuipitia Bajeti ya Ofisi hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kabla ya kuanza kutoa maoni ya Kamati, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza Wajumbe wa kamati hii kwa uwezo na umahiri wao mkubwa wa kuelewa majukumu yao ya uongozi katika kipindi chote cha kufatilia bajeti za Wizara hii pamoja na kazi kubwa waliyoifanya ya kupitia, kuchambua na hatimae kuipitisha bajeti ya (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** Sasa kwa niaba ya Kamati yangu napenda kuwatambua Wajumbe waliounda Kamati hii kama ifuatavyo: -

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Machano Othman Said | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Mtumwa Peya Yussuf | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Suleiman Makame Ali | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Mohammed Mgaza Jecha | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Zaina Abdalla Salum | Mjumbe |
| 7. | Ndg. Mwanaisha Mohammed Kheir | Katibu |
| 8. | Ndg. Ali Alawy Ali | Katibu |
| 9. | Ndg. Amina Abeid Hemed | Mkalimani |

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya utangulizi huo kwa ruhsa yako na kwa mujibu wa Kanuni ya 97 (1) na 107(3) katika jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi ya Toleo la mwaka 2020, sasa naomba kutoa maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi

kuhusu bajeti ya (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2023/2024.

**Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora katika kufuatilia na kufanyia kazi Bajeti yake, inasimamia jumla ya Mafungu *Kumi na Tatu (13)* na Programu Kumi na Sita (16) ambazo zinatekelezwa chini ya Idara na Taasisi zinazojitegemea. Mafungu hayo ni kutoka Fungu G01 – Ofisi Kuu; Fungu G02 – Mahakama Kuu Zanzibar; Fungu G03 – Afisi ya Mwanasheria Mkuu; Fungu G04 – Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka; na Fungu G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria;

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, kwa upande wa Fungu E04, E05, E07 na E08 yanasimamiwa na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi; Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali; Kamisheni ya Utumishi wa Umma na Tume ya Utumishi Serikalini;

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Fungu G12 mpaka G15 yanasimamiwa na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana; Wakala wa Serikali Mtandao; Afisi ya Mufti Mkuu na Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Hata hivyo, Kamati yetu haikujadili Fungu la Ofisi ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwa vile fungu hilo lilipitiwa na Kamati ya PAC.

**Mheshimiwa Spika,** Katika Fungu **G01** la Ofisi Kuu, Kamati inapenda kuipongeza (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kwa jitihada kubwa wanazozifanya katika utekelezaji wa majukumu yao ya kila siku, jitihada ambazo zinaonekana kuzaa matunda, kwani zimekua zikiwasaidia wananchi na Serikali kupitia huduma mbali mbali wanazotoa kutoka idara na taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Kamati inawaomba kuendelea na moyo wa kuwatumikia wananchi na kujenga Nchi kwa faida ya Nchi na vizazi vijavyo.

**Mheshimiwa Spika,** kuhusu taasisi zinazopewa ruzuku kupitia Ofisi Kuu, Kamati inashauri kupitia **Kifungu PG0105** *Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi* kwa Chuo cha Utawala wa Umma kuharakisha upatikanaji wa kiwanja kipya baada ya Kamati kushauri kuzuiwa ujenzi wa kiwanja cha mwanzo. Aidha, tunaomba chuo cha IPA kusimamia mipango yao ya kuendeleza kutoa mafunzo ya kujenga uwezo wa watumishi wa Umma pamoja na kutoa mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa wakati na kwa kuzingatia maadili na mifumo ya uwajibikaji.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Skuli ya Sheria Zanzibar; Kamati inaipongeza kwa kuzipatia mafunzo ya vitendo Taasisi za Serikali ikiwemo ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Mahkama Kuu Zanzibar, Ofisi ya Mkurugenzi Mashtaka na Sekta binafsi. Hata hivyo, Kamati inaendelea kuishauri Serikali kufanya haraka katika suala la kuipatia Skuli ya Sheria jengo la kudumu kwa ajili ya kuendesha kazi zake.

**Mheshimiwa Spika,** katika Kifungu cha **PG0201** programu kuu ya *Usimamizi wa Upatikanaji wa Haki* ambayo inasimamiwa na Mahkama Kuu Zanzibar; imepangiwa kutumia jumla ya TSH. Bilioni 25 kwa ajili ya Mradi wa Ujenzi wa Mahakama za Mkoa wa Kaskazini Pemba, Mkoa wa Mjini Magharibi na Mkoa wa Kaskazini Unguja. Kutokana na hali mbaya za Mahakama za Mikoa na Wilaya, Kamati yangu inaishauri Serikali kuangalia kwa umakini suala hili na kuhakikisha Mahakama hizi zinajengwa kupitia fedha hizi kama zilivyokusudiwa.

**Mheshimwa Spika,** Aidha, Kamati inaitaka Mahakama kupitia mradi wa Kuanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Taarifa za Kesi (ECMICS) ambapo jumla ya TSH. Bilioni 2 zimetengwa kwa lengo la kuanzisha mfumo huu na kuendesha kesi kwa njia ya kisasa ambayo inapunguza changamoto

nyingi ikiwemo rasilimali watu na pia, inapunguza mrundikano wa kesi katika Mahakama zetu. Kamati, inaomba Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kuhakikisha fedha hizo zimepatikana ili kwenda sambamba na malengo yaliyokusudiwa. Sambamba na hayo, Kamati inaitaka (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuhakikisha wanasimamia mradi huu katika hatua zote kwani utendaji wake unaendelea, sambamba na kutafutia ufumbuzi kilio cha muda mrefu cha watendaji kwa kumaliza changamoto ya usafiri pamoja na vitendea kazi kwa Mahkama zetu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati kupitia **Fungu G03,** inaipongeza Afisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa mafanikio makubwa waliyopata katika programu zao walizotekeleza kwa mwaka wa fedha 2022/2023. Hata hivyo, kupitia Bajeti ya mwaka 2023/2024 Kamati inashauri Afisi ya Mwanasheria Mkuu kupitia Programu Ndogo ya Ubora na Ufanisi wa Huduma za Kisheria; kuhakikisha huduma za kutoa ushauri wa kisheria juu ya Mikataba ya Serikali ya kikanda na kimataifa ambayo wanaisimamia kuhakikisha utekelezaji wake unakwenda sambamba na malengo ya nchi kwa kukuza na kuboresha maendeleo na sio kuitia hasara Serikali kupitia Mikataba hiyo. Pia, Kamati yangu inaiomba Afisi ya Mwanasheria Mkuu kukaa na Maafisa wa sheria wa Wizara na Taasisi za Umma zinazohusika na masuala ya Mikataba ili kutoa elimu inayofaa kulingana na Mikataba wanayoandika.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka yenye **Fungu G04** Kamati inaomba kuendeleza na kuongeza taaluma mahsusi kwa Waendesha Mashtaka na Wapelelezi kuhusu makosa ya udhalilishaji na uhalifu ili mashauri hayo yaweze kufanyiwa kazi kwa wakati na ufanisi. Sambamba na hilo, Kamati inaitaka (OR) Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora kuliangalia jengo kongwe linalojuilikana kama Nyumba ya Miguu liliopo mkabala na Mahakama ya Wete ambapo ofisi ya DPP wanataka kulifanyia matengenezo kwa ajili ya Matumizi ya Ofisi ya Mwendesha Mashtaka Mkoa wa

Kaskazini Pemba, Kamati inashauri jengo hili kulivunja na kujenga ofisi mpya kutokana na muonekano wa jengo hilo kuhitaji fedha nyingi sana ambazo zitaigharimu Serikali bila ya kuwepo uhakika wa matumizi ya jengo hilo kwa muda mrefu ujao.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2022/2023 Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar yenye **Fungu G05** ambayo inasimamia Programu Kuu ya Kufanya Mapitio ya Sheria; pamoja na mambo mengine, Kamati imebaini kuwa programu hii ilikabiliwa na changamoto ya uhaba wa fedha na hivyo kupelekea uwepo wa Taasisi nyingi zenye Sheria zenye mapungufu na zinazohitaji kufanyiwa mapitio na hatimae kurekebishwa. Hivyo basi, kwa mwaka 2023/2024 Kamati inaiomba Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuiangalia kwa jicho la huruma Tume hii na kuwapatia fedha za matumizi kwa wakati muafaka ili waweze kutimiza malengo yao.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaiomba Tume kuipitia kwa umakini sheria Namba 2 ya Mwaka 2011 Sheria ya Utumishi wa Umma ambayo inatarajiwa kufanyiwa marekebisho katika vipengele mbali mbali ikiwemo suala la nidhamu za watumishi na kadhalika. Aidha, Kamati inaiomba Serikali kulipa umuhimu suala la ujenzi wa ofisi mpya ya Tume ya Kurekebisha Sheria kwa kuwa jengo la hivi sasa halina nafasi ya kutosha na halina afya njema kwa watendaji wake.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi kwa kuelekeza nguvu zao katika udhibiti wa vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi kwa kuhakikisha fedha za Serikali zinatumika kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa. Kupitia program ndogo ya **SE050101** ya kupunguza Matendo ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi; Kamati inaiomba Serikali kuwapatia mgao wa fedha Mamlaka hiyo ili kurahisisha operesheni zao

kwa kuwa Mamlaka hii inaingiza fedha nyingi Serikalini zinazotokana na ukamataji wanaoufanya.

**Mheshimiwa Spika,** katika **Fungu E07** Kamati inaipongeza Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa kuidhinisha Miundo ya Taasisi za Umma 20 sambamba na kufanya ufatiliaji wa utekelezaji wa Miundo hiyo kwa taasisi za Serikali kwa kuzipitia Wizara zote 18 za Unguja na Pemba kwa kipindi cha Julai 2022 hadi kufikia Machi 2023. Hata hivyo, tunawaomba waendelee na utaratibu wa kufanya ukaguzi kwa Taasisi zote za Zanzibar na kufanya tathmini ya utekelezaji wa Miundo ya Taasisi za Umma ambazo miundo yao imeidhinishwa na Kamisheni.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaishauri Kamisheni ya Utumishi wa Umma kupitia Programu Ndogo ya **SE070102** ya *Usimamizi wa Nidhamu na Maadili katika Utumishi wa Umma;* kufanya ziara katika taasisi za umma kwa ajili ya kutoa elimu kwa wafanyakazi pamoja na kuwachukulia hatua wale wote wasiofuata Miundo ya Taasisi zao ambayo imeidhinishwa kisheria na hivyo, kupelekea baadhi ya watendaji kukosa haki na fursa zao kwa mujibu wa taratibu za nchi.

**Mheshimiwa Spika,** kupitia programu za **Fungu G12** Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Zanzibar; sote tunafahamu kuwa Kamisheni hii ipo kwa ajili ya kuendeleza mali za wakfu na Amana kwa Wananchi wetu wa Zanzibar ili waweze kunufaika na huduma hizo. Hata hivyo, Kamati inaiomba Kamisheni kuzidi kusaidia na kuimarisha mikakati ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia Zakka, Sadaka na Misaada ya kheri inayotolewa na jumuiya na taasisi mbali mbali ndani na nje ya nchi. Aidha, Kamati inashauri Serikali kupitia Programu Ndogo ya **SG1202** ya Utawala na Uendeshaji wa Ofisi; kuzidisha kasi ya kuiwezesha Kamisheni kujiendesha katika masuala ya kiuchumi kwa kupatiwa wataalamu wa kuwekeza katika mitaji mikubwa ya kifedha kama

zilivyo nchi nyengine za Kiislamu. Kamati inaiomba Serikali kuharakisha Mchakato wa kuanzisha akaunti maalum kwa mahitaji toka Zanzibar ili kupunguza usumbufu kwa vile Muundo wa sasa wa mahujaji wote wa Tanzania kuwa na akaunti moja unawakwaza mahujaji wetu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Wakala wa Serikali Mtandao yenye **Fungu G13** Kamati inawataka kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kuharakisa mapitio ya Sera ya serikali Mtandao ya Mwaka 2012 ili iweze kwenda sambamba na mabadiliko ya sasa katika suala zima la utumiaji wa mifumo ya TEHAMA. Sambamba na hilo, Kamati haikuridhishwa na mwenendo wa sasa kwa baadhi ya mifumo kama vile Mfumo wa maombi ya ajira ambao unatumiwa na Tume ya Utumishi Serekalini kwa ajili ya kufanya maombi ya ajira na taratibu zote zinafanyika kupitia njia ya mtandao.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na changamoto nyingi za mfumo huu ambazo bado zinaleta usumbufu kwa waombaji, Kamati inashauri Wakala kufanya juhudi za haraka na kitaalamu zaidi kuhakikisha mfumo huu unafanya kazi kwa mujibu wa malengo yaliyokusudiwa. Aidha, Wakala ihakikishe malengo yaliyowekwa katika programu ya Huduma za Serikali Mtandao yametekelezwa kama yalivyopangwa kwa mujibu wa upatikanaji wa fedha.

**Mheshimiwa Spika,** katika **Fungu G14** – Afisi ya Mufti Mkuu Zanzibar; Kamati inaipongeza Ofisi ya Mufti Mkuu kutokana na mpangilio wa kazi zao wanazozifanya zikiwemo shughuli za kuandama kwa mwezi pamoja matayarisho ya Baraza la Eid. Kamati yangu inaiomba Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumimshi na Utawala Bora kuangalia umuhimu wa Ofisi hii kupata eneo lake la kujenga Ofisi ya Kudumu kwa upande wa Pemba ambayo itawasaidia kupata sehemu ya kutosha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi. Kamati inampongeza sana katibu mtendaji Ofisi ya Mufti kwa Kusimamia vyema majukumu ya ofisi hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma ina jukumu kubwa la kuhakiki taarifa za mali na madeni za viongozi wa umma na kupokea na kusikiliza na kutoa maamuzi kuhusu malalamiko na madai ya uvunjaji wa maadili ya viongozi wa umma. Kupitia programu ndogo ya **SG150101** ya *Usimamizi wa Maadili ya Viongozi wa Umma,* Kamati inaitaka Wizara kuwachukulia hatua za kinidhamu viongozi wote ambao huitwa kwa ajili ya kuhojiwa juu ya malalamiko na kutoa vitisho kwa watendaji wao ambao huitwa kwa ajili ya kutoa ushahidi kwani kufanya hivyo ni kuendelea kuvunja maadili ya viongozi.

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande mwengine kamati iniomba Serikali kuongeza watumishi katika Tume hiyo katika fani na kada za Sheria, Uchunguzi na Mipango ili kuongeza nguvu za utendaji katika kazi zao.

**HITIMISHO:**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaitaka Wizara kwa mwaka wa fedha ujao wa 2023/2024 kuweka jitihada zaidi katika kutekeleza majukumu yake ili manufaa yaliyokusudiwa yaweze kupatikana kwa Serikali na Nchi kwa ujumla. Sambamba na hayo, Kamati inaiomba Serikali iwapo hali ya fedha itaruhusu, iongezewe fedha za miradi ya maendeleo ili iweze kutekeleza miradi hiyo kwa wakati kwani changamoto zote zilizopo haziwezi kutatuka bila ya kuwa na fedha za kutosha za kuendeshea shughuli zao.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati imeona kwamba majukumu mengi ya taasisi za Serikali hayawezi kufanyika ipasavyo kutokana na kutoingizwa fedha kwa wakati na kwa mujibu wa kilichopangwa katika bajeti zao. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuingiza fedha kwa wakati na kama ilivyokusudiwa ili

ufanisi wa kiutendaji uweze kupatikana kwa maendeleo ya wananchi na nchi yetu kwa ujumla.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kumalizia, naomba kukushukuru tena kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa katika Baraza lako Tukufu. Pia, niwashukuru Wajumbe kwa kunisikiliza kwa utulivu wakati wa kuwasilisha Hotuba hii, na ninawaomba waichambue, waichangie na hatimae waipitishe bajeti ya mwaka wa fedha 2023/2024 kwa Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora ili wakaweze kutekeleza shughuli zote zilizokusudiwa kwa mwaka huu.

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Kamati yangu;

***Naomba Kuunga Mkono Hoja.***

Ahsante,

……………………………………

(Mhe. Machano Othman Said)

**Mwenyekiti,**

***Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,***

**BARAZA LA WAWAKILISHI**,

**ZANZIBAR**